


TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZA MUDA WA UDAHILI KWA VYUO NA PROGRAMU AMBAZO BADO ZINA NAFASI KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

1.0. Utangulizi

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania inautangazia umma kuwa udahili katika awamu zote tatu kwa mwaka wa masomo 2019/2020 umekamilika kwa mujibu wa ratiba ya udahili iliyoidhinishwa.

2.0. Mwenendo wa Udahili

Jumla ya waombaji **96,338** walituma maombi katika awamu zote tatu kwa vyuo **75** vilivyoruhusiwa kudahili kwa mwaka wa masomo 2019/2020. Waombaji **82,758** sawa na asilima **85.9** wamedahiliwa katika vyuo hivyo. Kati ya hao, waombaji **37,450** sawa na asilimia **45** ya wadahiliwa wote, walidahiliwa na zaidi ya chuo kimoja. Mpaka sasa waombaji **33,453** sawa na asilimia **89.3** wameshajithibitisha katika chuo kimoja, na wengine wanaendelea kujithibitisha hadi tarehe 30/09/2019. Tume inaendelea kuwasisitiza waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja ambao bado hawajajithibitisha, wathibitisha katika vyuo wanavyopenda kusoma mapema iwezekanavyo ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.

3.0. Kufunguliwa kwa Dirisha la Udahili Awamu ya Nne

Baada ya kukamilika kwa awamu zote tatu za udahili, Tume imeendelea kupokea maombi ya kuongezwa muda wa udahili kutoka kwa baadhi ya waombaji wa udahili ambao hawakupata udahili kutokana na sababu mbalimbali. Aidha Tume imepokea maombi ya kuongezwa muda wa udahili kutoka kwa baadhi ya vyo vya ambavyo bado vinazo nafasi za udahili katika baadhi ya programu za masomo kwa mwaka 2019/2020.

Ili kutoa fursa kwa wananchi ambao ama hawakuweza kudahiliwa au hawakuweza kuomba udahili katika awamu tatu zilizopita, na kwa kuzingatia maombi ya baadhi ya vyo kwamba bado wanazo nafasi za udahili, Tume imeongeza muda wa udahili kwa kufungua dirisha la awamu ya nne itakayoanza tarehe **01** hadi **04 Oktoba, 2019**.

4.0. Wito kwa Vyo vya Elimu ya Juu

Tume inatoa wito kwa vyo vyote vye elimu ya juu kubainisha programu zenye nafasi ili kuwawezesha waombaji kufanya maamuzi sahihi wakati wa kutuma maombi ya udahili na kuepusha usumbufu kwa waombaji kuomba programu ambazo hazina nafasi.

Aidha Tume **inasisitiza** vyo vyote kuzingatia idadi ya wanafunzi iliyoidhinishwa katika programu husika.

5.0. Wito kwa Waombaji wa Udahili

Waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili ama kujithibitisha yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyo husika na siyo TCU. Kwa wale ambao wana changamoto katika kujithibitisha, vyo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

KATIBU MTENDAJI

25 Septemba, 2019